



# *Muhtasari wa Mwenendo wa Mvua kwa Siku 10 Zilizopita na Matarajio kwa siku 10 Zijazo*

## **1.0 MUHTASARI WA MWENENDO WA MVUA KWA TAREHE 21-31 JANUARI, 2025 NA MATARAJIO YA MVUA KWA TAREHE 01-10 FEBRUARI, 2025**

### **1.1 MUHTASARI WA MWENENDO WA VIASHIRIA NA MIFUMO YA MVUA KWA TAREHE 21-31 JANUARI, 2025**

Katika kipindi hiki, migandamizo mikubwa ya hewa iliyopo kusini mwa dunia (St. Helena na Mascarene) iliendelea kudhoofika wakati ile iliyopo kaskazini mwa dunia (Azore na Siberia) iliendelea kuimarika. Hali hii ilidumisha mwenendo wa sehemu ya ukandamvua (ITCZ) kuelekea kusini na kuwepo katika maeneo ya magharibi mwa nchi yetu, nyanda za juu kusini magharibi, kati na maene ya kusini mwa nchi. Kwa upande mwingine joto la bahari katika eneo la magharibi mwa bahari ya Hindi (pwani ya Afrika Mashariki) lilikuwa la juu kidogo ya wastani. Hali hii ilichangia katika kuimarisha mifumo isababishayo mvua katika maeneo ya ukanda wa pwani na nyanda za juu kaskazini mashariki mwa nchi yetu.

### **1.2 MUHTASARI WA MWENENDO WA MVUA KWA TAREHE 21-31 JANUARI, 2025**

Viashiria vilivyotajwa hapo juu vilipelekea kuwepo kwa mvua na ngurumo za radi katika maeneo machache ya magharibi mwa nchi, nyanda za juu kusini magharibi, kusini mwa nchi ukanda wa ziwa victoria na nyanda za juu kaskazini mashariki. Vilevile vipindi vya mvua viliripotiwa katika maeneo machache ya maeneo ya ukanda wa Pwani na na maeneo ya kati mwa nchi.

## **2.0 MATARAJIO YA HALI YA HEWA KWA TAREHE 01-10 FEBRUARI, 2025**

### **2.1 VIASHIRIA NA MIFUMO YA MVUA KWA TAREHE 01-10 FEBRUARI, 2025**

Katika kipindi hiki, migandamizo mikubwa ya hewa iliyopo kusini mwa dunia (St. Helena na Mascarene) inatarajiwa kuendelea kudhoofika wakati ile iliyopo kaskazini mwa dunia (Azore na Siberia) inatarajiwa kuendelea kuimarika. Hali hii inatarajiwa kuendelea kudumisha mwenendo wa sehemu ya ukandamvua (ITCZ) kuelekea kusini na kuwepo katika maeneo ya magharibi mwa nchi yetu, nyanda za juu kusini magharibi, kati na kusini. Kwa upande mwingine joto la bahari katika eneo la magharibi mwa bahari ya Hindi (pwani ya Afrika Mashariki) linatarajiwa kuwa la juu kidogo ya wastani. Hali hii inatarajiwa kuimarisha mifumo isababishayo mvua katika baadhi ya maeneo ya ukanda wa pwani na maeneo jirani.

*Mawasiliano yote yaelekezwe kwa:*

Mkurugenzi Mkuu, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania, Chuo Kikuu cha Dodoma,  
Jengo la Utawala, Ndaki ya Sayansi za Kompyuta na Elimu Angavu, 1 Mtaa wa CIVE,  
S.L.P 27, 41218 Dodoma; Simu: +255 26 2962610; Nukushi: +255 26 2962610  
Barua pepe; [met@meteo.go.tz](mailto:met@meteo.go.tz); Tovuti: [www.meteo.go.tz](http://www.meteo.go.tz)

## **2.2 MWELEKEO WA MVUA KWA TAREHE 01-10 FEBRUARI, 2025**

**Kanda ya ziwa Viktoria (Mikoa ya Kagera, Geita, Shinyanga, Mwanza, Simiyu na Mara):** Ngurumo za radi zinatarajiwa katika maeneo machache.

**Nyanda za juu kaskazini-mashariki (Mikoa ya Arusha, Manyara na Kilimanjaro):** Hali ya ukavu kwa ujumla inatarajiwa.

**Pwani ya kaskazini (Mikoa ya Tanga, Maeneo ya kaskazini mwa Morogoro, Pwani na Dar es Salaam pamoja na visiwa vya Unguja na Pemba):** Vipindi vya mvua vinatarajiwa katika maeneo machache.

**Magharibi mwa nchi (Mikoa ya Kigoma, Katavi na Tabora):** Mvua zinazoambatana na ngurumo za radi zinatarajiwa katika katika maeneo machache.

**Kanda ya kati (Mikoa ya Dodoma na Singida):** Vipindi vya mvua vinatarajiwa katika maeneo machache.

**Nyanda za juu Kusini-magharibi (Mikoa ya Rukwa, Songwe, Mbeya, Njombe na Iringa):** Mvua zinazoambatana na ngurumo za radi zinatarajiwa katika maeneo machache.

**Pwani ya kusini (Mikoa ya Mtwara na Lindi):** Mvua zinazoambatana na ngurumo za radi zinatarajiwa katika maeneo machache.

**Kanda ya kusini (Mkoa wa Ruvuma na Maeneo ya kusini mwa Morogoro):** Mvua zinazoambatana na ngurumo za radi zinatarajiwa katika maeneo machache.

Imetolewa na;

### **MAMLAKA YA HALI YA HEWA TANZANIA**

---

*Mawasiliano yote yaelekezwe kwa:*

Mkurugenzi Mkuu, Mamlaka ya Hali ya Hewa Tanzania, Chuo Kikuu cha Dodoma,  
Jengo la Utawala, Ndaki ya Sayansi za Kompyuta na Elimu Angavu, 1 Mtaa wa CIVE,  
S.L.P 27, 41218 Dodoma; Simu: +255 26 2962610; Nukushi: +255 26 2962610  
Barua pepe; [met@meteo.go.tz](mailto:met@meteo.go.tz); Tovuti: [www.meteo.go.tz](http://www.meteo.go.tz)